

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI


MKOA WA MBEYA

Simu ya Mdomo: 252957440/252957447

Fax: 025-2590089/2590108

Baruazoteziandikwekwa

MkurugenziMtendaji (W) Mbarali



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 237,

RUJEWANA.

KITENGO CHA SHERIA

1.0 UTANGULIZI

Kitengo cha sheria ni moja ya vitengo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na lengo kuu la kitengo hiki ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria na kusimamia kesi zinazoihusu Halmashauri.

2.0 MAWASILIANO YA KITENGO CHA SHERIA

SN	JINA	CHEO	NAMBA YA SIMU
1	Mr. Komba	Mkuu wa Kitengo cha Sheria	+255767422164
2	Fortunatus Mwandu	Mwanasheria	+255786754631

3.0 KAZI ZA KITENGO

- 1) Kusimamia na kutoa mafunzo katika mabaraza ya kata katika utatuzi wa migogoro ya ardhi na utoaji haki kwa mabaraza hivyo kufanikisha kutolewa kwa maamuzi yenye tija.
- 2) Kupitia mikataba mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na kutoa ushauri wa kuiboresha inapobidi
- 3) Kutoa elimu juu ya kodi mbalimbali na ushuru unaotazwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa wananchi, wenyeviti wa mitaa na vitongoji, watendaji wa kata na Waheshimiwa Madiwani hivyo kupelekea kuongeza mapato ya Halmashauri.

- 4) Kusimamia sharia ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa kushirikiana na Idara nyingine na hivyo kuleta tija na kuongeza mapato ya Halmashauri.
- 5) Kuiwakilisha Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika mashauri mbalimbali mahakamani. Halmashauri inapokea mashauri mbalimbali ambayo baadhi bado yanaendelea mahakamani na mengine yameshatolewa maamuzi.

4.0 HUDUMA ZINAZOTOLEWA KATIKA KITENGO CHA SHERIA

Kitengo hiki endapo mwananchi atakitembelea atapata huduma mbalimbali ikiwemo.

- 1) Kutoa ushauri wa kisheria kwa jamii pale panapokuwa na uhitaji ili kupunguza migogoro miongoni mwa jamii
- 2) Kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kufuata na kuzingatia sheria ndogo zilizotungwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa ushirikiano wa wananchi wenyewe.

5.0 MATARAJIO YA IDARA

Kitengo kinatarajia kufanya yafuatayo kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19

- 1) Kuongezaufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na jamii nzima kwa ujumla ili kupunguza migogoro isiyo ya lazima.
- 2) Kutoa miongozo ya kisheria kwa mabaraza ya kata ili kupunguza changamoto za kisheria katika mabaraza.